# MUHTASARI WA RIPOTI YA ALMA - ROBO YA KWANZA, 2025


## UTANGULIZI:

Mheshimiwa Rais João Lourenço wa Angola, akikubali nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika kwa mwaka huu, na amejitoa kushughulikia changamoto zinazohusiana na magonjwa na afya ya umma, ikiwa ni pamoja na kuunganisha juhudi za Afrika katika kutafuta ufumbuzi wa pamoja.

Hili ni muhimu hasa katika mapambano dhidi ya malaria; ambapo viwango vya maambukizo na vifo vinaongezeka kwa kiwango cha kutisha, vinavyotokana na dhoruba kamili ya changamoto; usugu wa viuatilifu na usugu wa dawa za kutibu malaria, kuongezeka maeneo ya mazalia ya mbu kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, mapengo makubwa ya ufadhili ambayo yameongezeka kutokana na kupungua kwa misaada ya maendeleo kwa nchi zinazoendelea – ODA.


**WANACHAMA**
Algeria
Angola
Benin
Botswana
Burkina Faso
Burundi
Cameroon
Central African Republic
Cabo Verde
Chad
Comoros
Republic of Congo
Côte d'Ivoire
Democratic Republic of Congo
Djibouti
Egypt
Equatorial Guinea
Eritrea
Eswatini
Ethiopia
Gabon
Ghana
Guinea
Guinea Bissau
Kenya
Lesotho
Liberia
Libya
Madagascar
Malawi
Mali
Mauritania
Mauritius
Mozambique
Morocco
Namibia
Niger
Nigeria
Rwanda
Sahrawi Arab Democratic Republic
São Tomé and Príncipe
Senegal
Seychelles
Sierra Leone
Somalia
South Africa
South Sudan
Sudan
The Gambia
Togo
Tunisia
Uganda
United Republic of Tanzania
Zambia
Zimbabwe

**% ya Mpango Mkakati wa Malaria uliopata Ufadhili. (2024-2026)**




**Chanzo: Robo ya 1, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA.**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.*

**Aina ya viuadudu vyenye usugu wa mbu vilivyothibitishwa toka mwaka 2010**




**Chanzo: Robo ya 1, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA.**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.*

Mwenyekiti wa ALMA; Rais Wakili Duma Gideon Boko alitoa wito kuchukua hatua ya utekelezaji wa pamoja. "Afrika lazima ikabiliane na changamoto hiyo haraka kwa kuhamasisha rasilimali toka vyanzo vya ndani, ikijumuisha matumizi ya rasilimali toka mifuko yetu ya dharura na kuongeza mgao wa bajeti ya afya. Ni lazima pia kuongeza ufadhili wa kibunifu ikiwa pamoja na kupitia mabaraza na mifuko ya fedha za kutokomeza malaria, na kuimarisha majukwaa kama Benki ya Dunia - Jumuiya ya Maendeleo ya


Kimataifa na Mfuko wa hali ya hewa ya kijani, ili kuhakikisha kwamba programu zetu za kitaifa zina vifaa kikamilifu vya kuendeleza mbele ajenda ya malaria.”

Katika kilele cha Mkutano wa Umoja wa Afrika, Mheshimiwa Rais Wakili Duma Gideon Boko alizindua sura mpya ya kampeni ya *Badilisha Hadithi* ambayo inaweka sauti za watoto katika kiini cha mapambano ya malaria. Kampeni hiyo inalenga kuhamasisha nchi wafadhili na zilizoathirika kuongeza msaada wao kwa afua za kupambana na malaria, ikiwa ni pamoja na zana mpya na zenye nguvu, kupitia kuhamasisha rasilimali. Sura mpya iliangazia hadithi za watoto kutoka Msumbiji, Nigeria na Rwanda, ambazo zinazoonesha athari zinazotokana na hali mbaya ya hewa, jinsi ugonjwa huo unavyoathiri watoto na zana mpya za ubunifu ambazo zinaweza kusaidia kuushinda ugonjwa huo. Kampeni hiyo ilikuzwa zaidi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani mnamo Aprili 2025, wakati video ya kampeni ilichezwa kwenye televisheni ya kitaifa huko Eswatini, Ghana, Nigeria na Uganda, na kuwafikia zaidi ya watu milioni 70. Kampeni hii inalenga kuangazia kwamba ni taifa lililo hatarini zaidi na ambalo ni mtaji muhimu zaidi wa kibinadamu ambao unarudishwa nyuma na uwekezaji duni wa sasa katika mapambano dhidi ya malaria.

**MAJIBU YALIYOJIRI:**

Katika maadhimisho ya siku ya malaria duniani, wadau kote barani Afrika walikubali kaulimbiu: "Malaria inamalizwa na sisi. Wekeza Upya, Fikiria Upya, Washa Upya." Kwa hakika nchi mbili katika bara hili, Burkina Faso na Liberia, zilizindua mabaraza na mifuko ya kutokomeza malaria na kushirikisha sekta na wadau mbalimbali ili kuwashirikisha viongozi katika nchi hizi na kuanzisha mifumo ya kitaifa ya ufadhili wa sekta binafsi ili kuongeza mgao wa bajeti kwa sekta ya umma.  Barani Afrika, Mabaraza ya kutokomeza malaria yamekusanya zaidi ya Dola za Marekani minilioni150  kutoka sekta ya umma na sekta binafsi hadi sasa.

**Mabaraza na Mifuko ya Kutokomeza Malaria na Magonjwa ya Kitropiki ambayo Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele.**





**Chanzo**:  **Robo ya 1, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA**.

*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu  uwekaji mipaka au mipaka yake.*


Katika bara lote, kulikuwa na mkazo kwa akina mama, watoto, na vijana kama makundi ya watu yaliyoathiriwa moja kwa moja na janga hili. Kwa kuzingatia kampeni ya badilisha hadithi (ushirikiano wa utetezi kati ya ALMA, Shirika la Kumaliza Malaria la Uingereza na Ushirikiano wa Kudhibiti Malaria - RBM). Watoto wa shule walitoa hotuba kwa umma, na kuonesha uelewa wao wa sayansi ya malaria na mpangilio mzuri wa masomo ya darasani.

**% ya Ugawaji wa dawa kwa Jamii kufikia malengo ya Shirika la Afya Duniani**




**Chanzo: Robo ya 1, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA.**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.*

**Huduma ya Matibabu kwa Jamii kwa magonjwa ya Kitropiki ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele (NTD index, %) (2023)**




**Chanzo: Robo ya 1, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA.**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka*

## KUWEKA MALARIA KUWA AGENDA KUU:

Mawaziri wa bara la Afrika wamechukua jukumu la kuwa mabingwa wa ugonjwa wa Malaria, ili kuharakisha maendeleo ya kutokomeza Malaria. Wanaoongoza ni Mawaziri kutoka Botswana, Burkina Faso, Equatorial Guinea, Malawi, Msumbiji, Uganda na Zimbabwe.


Waliwaalika mawaziri wengine kujiunga na shughuli zao kwa ukubwa, mawaziri wamejitoa ili:

- Kuweka kipaumbele katika kutokomeza malaria nchini mwao kwa kuzindua Kampeni ya Ziro Malaria inaanza na Mimi, kuendeleza programu za kisekta za malaria pamoja na elimu, mazingira, kilimo na sekta nyinginezo muhimu; wakiwemo wabunge, vijana, AZAKi, viongozi wa dini na viongozi wa jadi; kuanzisha mabaraza ya washikadau mbalimbali ya kutokomeza malaria.
- Kuimarisha ufadhili wa malaria kwa kuhimiza ongezeko la mgao wa bajeti, kuweka fedha za kutokomeza malaria ili kutumia rasilimali za sekta binafsi, kupitisha ufadhili wa kibunifu na kutetea ujumuishaji katika ajenda pana za maendeleo (k.m. Jumuiya

ya Maendeleo ya Kimataifa, ufadhili mseto, na ufadhili wa hali ya hewa).

Kujumuisha malaria katika Huduma ya Afya ya Msingi ikiwa ni pamoja na kuwapa kipaumbele wahudumu wa afya katika jamii, kujiandaa na janga la magonjwa na programu za kukabiliana na hali ya hewa ili kukabiliana na hali hiyo. Muunganisho kamili katika Huduma ya Afya ya Msingi ni muhimu ukawa endelevu.

**Kuelekea lengo la kupunguza matukio ya malaria angalau kwa 63% ifikapo mwaka 2023 (vs 2015)**





**Chanzo: Robo ya 1, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA.**

*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake*

- Kuimarisha ufuatiliaji wa takwimu kitaifa ikijumuisha ufuatiliaji wa genomiki na utekelezaji wa zana za kadi ya alama za nchi kwa uwajibikaji na ufuatiliaji ili kuleta athari. Shiriki kadi ya alama na takwimu kwenye kitovu cha kadi ya alama cha ALMA na dashibodi ya RBM. Kuimarisha programu za kidijitali za utabiri wa mahitaji na usimamizi wa mnyororo wa ugavi nchini kote.

**Uchunguzi wa ufanisi wa dawa uliofanywa tangu mwaka 2019 na takwimu kuripotiwa Shirika la Afya Duniani.**




**Chanzo: Robo ya 1, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA.**

*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.*

Uchunguzi wa mara kwa mara wa ufanisi wa dawa, pia ni muhimu kufuatilia usugu wa dawa na kuhakikisha hatua zinachukuliwa kwa wakati.

- Hakikisha utumiaji wa haraka wa zana na mbinu za kibunifu ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya uidhinishaji katika udhibiti, mafunzo kwa wafanyakazi na elimu kwa umma.
- Kuhudhuria matukio ya utetezi unaohusisha masuala ya malaria, mikutano na ujumbe maalum wa vikao vya kikanda na kimataifa.

**HITIMISHO:**

Vita dhidi ya malaria viko katika njia panda. Labda tushiriki katika vita vya kila aina au tupoteze mafanikio ambayo tumeyapata katika miongo 2 iliyopita. Sasa ni wakati wa msukumo mkubwa kushinda dhoruba kamili ya changamoto zinazotishia mapambano dhidi ya malaria kwa sasa.